

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



TANGAZO

MALIPO YA FIDIA KWA WAKAZI WALIOKO KWENYE ENEO LA MRADI WA UJENZI WA KITUO KIKUU KIPYA CHA MABASI MBEZI LUIS

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam anatarajia kufanya malipo ya fidia kwa wakazi 65 waliopo ndani ya eneo la mradi wa ujenzi wa kituo Kikuu kipya cha mabasi Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo.

Malipo haya yatafanyika mara tu mfumo wa malipo ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 utakapokuwa tayari.

Hivyo wahusika wote wanataarifiwa kujiandaa na kuandaa nyaraka zifuatazo:-

- (i) Picha mbili za rangi “colored passport size”.
- (ii) Kama eneo linalolipwa fidia ni mali ya urithi, itahitajika kuwasilishwe muhtasari wa kikao cha familia pamoja na barua ya usimamizi wa mirathi toka mahakamani.
- (iii) Kwa wenye maeneo ambayo yamefanyiwa upimaji na kumilikishwa kwa Hatimilki wanatakiwa warejeshe nyaraka hizo.
- (iv) Namba za Akaunti za Benki kwa ajili ya Uhakiki

Baada ya taratibu hizi kukamilika, malipo yatalipwa moja kwa moja kwenye akaunti zao walizowasilisha.

Imetolewa na.

Sipora J. Liana
Mkurugenzi wa Jiji
Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam